

Maswali

1. Nani alikuwa baba wa Yonathani?
2. Mbona Sauli alimuonea Daudi wivu?
3. Sauli alimfanyaje Daudi?
4. Yonathani alikuwa na ustadi gani?
5. Daudi na Yonathani walisikizana kwa ishara gani?
6. Sauli alifanyaje Yonathani?
7. Yonathani alirusha wapi mshale?
8. Ni maagano gani waliyofanya Daudi na Yonathani?
9. Daudi alimfanyia nini Yonathani alipokufa?
10. Nani ndiye rafiki wetu wa kweli?

Majibu

1. Sauli.
2. Wakati wakuimba watu walimsifu Daudi zaidi ya Sauli.
3. Alimtupia mkuki.
4. Alilinga vizuri mishale kwa upindi.
5. Kama Yonathani angerusha mishale karibu, kila kitu ni vyema. Akirusha mbali na Daudi, lazima asirudi.
6. Alimtupia mkuki.
7. Alirusha mbali na Daudi.
8. Daudi angekuwa mfalme; Yonathani angekuwa makamu wake.
9. Aliandika maombolezo na akafunza Waisraeli kutumia upindi na mishale.
10. Yesu ndiye rafiki wa kweli. Alijitoa kwa vyovyote kwa ajili yetu.

SHULE YA JUMAPILI YA CBM

Awamu ya 1 Mwaka wa 2



14 Daudi na Yonathani

Marejeo

1 Samweli 18, 19, 20

Kiini cha somo

Ni vizuri kuchagua marafiki wazuri maishani mwetu.

Maneno maalum

1. Goliathi + mwana wa mfalme + rafiki mzuri.
2. 1000 & 1000 + wivu + badilisha mawazo + rudi kwa sauli.
3. Wivu tena + muziki + mkuki + toroka.
4. Ogopa + kutana na Yonathani + karamu + mshale unapita Daudi.
5. Kasirika + mkuki + si mfalme + mshale unapita Daudi.
6. Windi Daudi + Kutana na Yonathani + maagano.
7. Maagano + Kufa + huzunika + omboleza + funza upindi na mishale.
8. Rafiki mzuri sana + Yesu + kila kitu + fanya anavyotaka.


14.1 Baada ya Daudi kuua Goliathi, alikaribishwa kukaa kwa nyumba ya mfalme Sauli. Mwana wa Sauli aitwaye Yonathani alishikana na Daudi wakawa marafiki wa karibu sana. Urafiki wao ulidumu kwa maisha yao yote.

14.2 Baadaye Waisraeli waliimba wimbo juu ya Sauli na Daudi. Walisema Sauli aliua elfu lakini Daudi ameua makumi elfu. Sauli aliona wivu na akataka kumuua Daudi. Yonathani kama rafiki mzuri alimhadharisha Daudi. Tena alimzungumzia babake ili ayageuze mawazo yake. Sauli akamkubali Daudi tena na akamrudisha kuishi nyumbani mwake.




14.3 Lakini baada ya mda mfupi Sauli akawa na wivu tena na akajaribu kumuua Daudi kwa mkuki alipokuwa akimchezea muziki. Daudi alihepa mkuki; akajua kwamba Sauli alinua kumuua na kumtoa kwa nyumba yake tena.

14.4 Daudi na Yonathani waliendelea kuwa marafiki; walikuwa na njia ya kuonana kwa siri. Daudi alitaka kurudi kwa nyumba ya Sauli lakini aliogopa chuki yake. Wakati wa karamu ulikaribia na Daudi lazima atakuwepo, Yonathani alimwambia Daudi kwamba atakuwa kwa hiyo karamu na atajua kama babake atamkubali Daudi. Walikubaliana vile atamjulisha nia ya babake. Yonathani aliwa na shabaha ya upindi. Angerusha mishale kwa shabaha, na hii ingeonyeshwa kwa kurusha mishale.



14.5 Wakati wa karamu Sauli aliuliza Yonathani juu ya Daudi, Yonathani alimwambia eti alikuwa ameenda nyumbani Bethlehemu. Sauli alikasirika na kumlinga mkuki, alimwambia kwamba yeye ndiye angekuwa mfalme baadaye lakini haitawezekana kama Daudi angali hai. Sauli hakusikiliza Mungu, Mungu aliwa aliwa ameambia Samweli kwamba Daudi ndiye atakayekuwa mfalme baadaye. Yonathani akaenda kutafuta Daudi, alirusha mshale ukapita alikokuwa Daudi. Hii ilikuwa ishara ya kuonyesha kwamba Daudi hakutakiwa kwa nyumba ya Sauli.



14.6 Rafiki walikutana tena. Sauli alitafuta kila pahali akitaka Daudi lakini hakumpata. Mungu alimkubali Yonathani kumfikia Daudi kwa urahisi. Wakafanya maagano. Daudi angekuwa mfalme wa Israeli na Yonathani atakuwa makamu wake.

14.7 Lakini haya hayakufanyika. Wakati wa vita na Wafiliti Sauli na Yonathani walikuwa. Daudi aliona vibaya na akaandika maombolezo juu yao. Alimpoteza rafiki mzuri. Baada ya haya Daudi alifunza jeshi la Israeli kutumia upindi na mshale. Hii ilikuwa namna ya kumkumbuka Yonathani.

14.8 Nani ndiye rafiki mzuri? Yesu alijitoa kwa vyovyote kwa ajili yetu hata uhai wake. Tena alisema tutakuwa rafiki zake ikiwa tutafanya anavyotaka. Yesu ndiye rafiki wa kweli.